JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



MUHTASARI WA MATOKEO YA TAFITI ZILIZOFANYWA NA OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO KWA MWAKA 2008/09

Umeandaliwa na:
Ofisi ya Rais,
Tume ya Mipango

Januari, 2010

YALIYOMO

UTANGULIZI.....i

1: 0 TATHIMINI YA UTEKELEZAJI WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025 1

1.1 Chimbuko 1

1.2 Malengo ya Tathimini 1

1.3 Matokeo ya Tathmini 1

1.4 Mapendekezoya Mtaalamu Mwelekezi.....3

1.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango.....5

2.0 KUAINISHA MAENEO YATAKAYOCHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI WA TANZANIA KULINGANA NA FURSA ZILIZOPO.....7

2.1 Chimbuko 7

2.2 Malengo.....7

2.3 Matokeo ya Utafiti.....7

2.4 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango.....10

3.0 UJUZI UNAOHITAJIKA KATIKA SOKO LA AJIRA KWENYE SEKTA ZA MADINI, UKARIMU NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO.....11

3.1 Chimbuko 11

3.2 Lengo la utafiti 11

3.3 Matokeo ya Utafiti.....12

3.4 Mapendekezo ya Mtaalamu Mwelekezi.....13

3.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango.....15

4.0 MFUMO WIANISHI WA USAFIRISHAJI KWA AJILI YA KUONGEZA UFANISI NA UKUAJI WA UCHUMI 17

.....17

4.1 Chimbuko 17

4.2 Malengo.....17

4.3 Matokeo ya Utafiti.....18

4.4 Mapendekezo yatokanayo na Utafiti 19

4.5 Maoni ya Tume ya Mipango 20

5.0 MCHANGO WA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA UCHUMI WA TAIFA22

5.1 Chimbuko 22

5.2 Lengo.....22

5.3 Matokeo ya Utafiti.....22

5.4 Mapendekezo yaliyotolewa na watafiti 23

5.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango.....24

UTANGULIZI

Katika mwaka wa kwanza wa kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango 2008/09, Tume iliibua maeneo kumi ya kufanyiwa utafiti na uchambuzi. Tafiti hizi zilifanywa na Wataalamu Elekezi kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Tume ya Mipango ambayo pia ilichambua matokeo ya tafiti hizi na kutoa mapendekezo yanayostahili kufanyiwa kazi na Serikali.

Taarifa hii inaelezea kwa muhtasari matokeo ya tafiti tano ambazo zimeshachambuliwa na Sekretarieti ya Tume ya Mipango. Tafiti hizo ni;

- Tathimini ya Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;
- Kuainisha Maeneo Yatakayochochea Ukuaji wa Uchumi Kulingana na Fursa Zilizopo;
- Ujuzi Unaohitajika katika Soko la Ajira kwenye Sekta za Madini, Ukarimu (hospitality); na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;
- Mfumo Wianishi wa Usafirishaji kwa Ajili ya Kuongeza Ufanisi na Ukuaji wa Uchumi; na
- Mchango wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Uchumi wa Taifa.

Kwa kila utafiti, muhtasari katika maeneo muhimu umetolewa. Muhtasari huo ni katika maeneo yafuatayo;

- Chimbuko la utafiti
- Malengo ya utafiti
- Matokeo yake
- Mapendekezo toka kwa mtaalamu mwelekezi; na
- Maoni ya Tume ya Mipango.

Taarifa ya kina ya uchambuzi wa maeneo haya kwa kila tafiti inapatikana katika Ripoti ya Wataalamu Elekezi iliyoambatanishwa.

1: 0 TATHIMINI YA UTEKELEZAJI WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025

1.1 Chimbuko

Kutokana na misukosuko ya kiuchumi iliyoikumba dunia pamoja na nchi yetu katika miaka ya 1980, Serikali iliona kuna umuhimu wa kuwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo itakayoongoza harakati za maendeleo ya kiuchumi na kijamii hadi mwaka 2025. Dira hiyo iliaandaliwa na kuanza kutekelezwa mwaka 2000. Malengo makuu matatu yaliyoainishwa kwenye Dira ni pamoja na:

- kuwaletea wananchi maisha bora;
- kudumisha uongozi bora na utawala wa sheria; na
- kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani.

Dira hii ilitegemewa kufanyiwa tathimini ya utekelezaji wake kila baada ya miaka mitano. Hata hivyo, tathimini hiyo haikufanyika kwa sababu Serikali ilijikita zaidi katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini ambayo ililenga pia katika kutekeleza Dira. Serikali imeona pia umuhimu bado upo wa kufanya tathimini ili kubaini hatua zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kama kuna haja ya kufanya marekebisho. Hivyo, Tume ya Mipango kwa kumtumia mtaalamu mwelekezi (Daima Associates Ltd) ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Dira Taifa ya Maendeleo 2025.

1.2 Malengo ya Tathimini

Lengo kuu ni kupima maendeleo yaliyofikiwa katika kufanikisha malengo yote 14 yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kutoa nafasi ya kubuni sera madhubuti za kiutendaji zitakazochochea maendeleo ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

1.3 Matokeo ya Tathmini

Matokeo ya tathimini yamebainisha kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 bado ni muhimu kwa Tanzania kwa sababu ni mwongozo pekee unaoonesha maendeleo ya Taifa ya muda mrefu, Taifa litakuwa wapi na matarajio ya wananchi kwa ujumla. Aidha, tathmini imeanisha mafanikio pamoja na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha miaka kumi ya utekelezaji wa

Dira.

Aidha, tathimini ilibainisha kuwa, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ni pamoja na:

i) Nchi kuwa na mwelekeo na falsafa ya maendeleo ya muda mrefu, tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya 1980 ambapo mipango yake ilikuwa ni ya mtazamo wa muda mfupi;

ii) Uchumi jumla umeendelea kutengamaa kama ifuatavyo:

- Wastani wa kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa miaka kumi iliyopita ulikuwa ni asilimia 6.2 (ikilinganishwa na lengo la malengo ya Dira ambacho ni ukuaji wa asilimia 8.0 au zaidi kwa mwaka);
- Kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei kutoka asilimia 39 mwaka 1999 hadi wastani wa tarakimu moja (single digit) katika kipindi cha 2000-2007; na;
- Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na kodi toka wastani wa Sh. 25 bilioni kwa mwezi; mwaka 1990/91 hadi Sh. 400 bilioni kwa mwezi; mwaka 2008/09.

iii) Huduma za elimu, maji, afya, chakula na lishe zimeboreshwa na maendeleo ni mazuri;

iv) Swala la utawala bora na wa kisheria limekua na kuimarishwa;

v) Mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi umeonyesha mafanikio katika ushirikishwaji wa wananchi kujikwamua kiuchumi na kuboresha maisha yao. Vile vile Mkakati wa Kurasimisha Biashara na Makazi Tanzania (MKURABITA) umeweza kuwasaidia wananchi wengi waliokuwa wanajishughulisha katika sekta isiyo rasmi.

Pamoja na mafanikio yaliyoainishwa hapo juu, tathimini imeonesha kuwa, zipo changamoto zilizojitokeza zikiwa ni pamoja na:

i) Kutokuwepo na chombo chenye jukumu la kuongoza na kusimamia utekelezaji wa Dira

ii) Kutokuwepo kwa mkakati wa kutangaza madhumuni ya Dira ya Taifa, kutafsiri malengo yake kimkakati katika utekelezaji wake.

iii) Kukosekana mipango ya muda wa kati ya kutekeleza Dira ya Maendeleo na tathmini yake;

iv) Jinsi ya kubadili kilimo kuwa cha kisasa, kuendeleza huduma na shughuli za viwanda na kuhimili ushindani wa kiuchumi;

v) Kutoainishwa kwa vigezo vya kupima viwango vya ushindani;

vi) Matumizi duni ya sayansi na teknolojia katika shughuli zote,

vii) Ukosefu wa uwiano katika kuwawezesha wananchi kiuchumi katika sekta zote,

viii) Kukosekana kwa sera za ushirikiano baina ya Sekta Binafsi na Umma (Public Private Partnership Policy); na

ix) Udhaifu wa jamii katika ubunifu na ugunduzi.

1.4 Mapendekezo ya Mtaalamu Mwelekezi

Kutokana na mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Dira, Wataalamu elekezi walipendekeza yafuatayo;

i) Dira ya Taifa itangazwe na ifahamike kwa upana zaidi. Wadau wote washirikishwe katika kuitangaza Dira ya Taifa na kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha malengo ya Dira ya Taifa yanafikiwa;

- Wanasiasa watangaze na kuhamasisha utekelezaji wa Dira katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku;
- Vitengo/idara zote zinazohusika na uenezaji habari (utoaji elimu) na mawasiliano katika wizara mbalimbali na taasisi zake vichukue nafasi ya kueneza habari zinazohusiana na Dira ya Taifa na utekelezaji wake; na
- Taasisi za elimu vikiwemo vyuo, vitoe elimu kuhusu malengo ya Dira ya Taifa kwa kufanya uchambuzi na kuangalia utekelezaji wake.

ii) Utekelezaji unatakiwa kuanza kwa kuibua mipango ya muda mrefu (2010 – 2025), ikiwa na malengo na shabaha zake, ikifuatiwa na mikakati ya muda mfupi itakayoendana na mipango ya muda mrefu. Dira ya Taifa na mipango yake ya muda mrefu itabainisha mahitaji (rasilimali) yatakayopelekea malengo ya Dira kufikiwa. Maeneo ya vipaumbele yanatakiwa yabainishwe kupitia fikra za kimaendeleo (strategic thinking);

iii) Kwamba swala la maendeleo ya taifa hayana budi yamlenge mwananchi na yatokane na ukuaji endelevu wa uchumi. Vile vile, jitihada za kuleta maendeleo zizingatie ushirikishwaji wa wadau wote na yalenge katika kutokomeza umaskini uliokithiri;

iv) Kwa kuzingatia umuhimu wa Dira ya Taifa, usimamazi na uratibu wa utekelezaji wake uendelee kuwa chini ya Tume ya Mipango katika Ofisi ya Rais ikiwa na mamlaka na uwezo wa kiutendaji katika kusimamia utekelezaji wake ikiongozwa na Rais, akisaidiwa na viongozi wengine katika ngazi mbalimbali serikalini na katika vyama vya siasa;

v) Umuhimu wa uwezeshaji kiuchumi katika kufanikisha mgawanyo sawa wa maendeleo yaliyopatikana, upatikanaji wa ajira kwa wingi na utulivu/amani katika mambo ya kisiasa ni vitu ambavyo serikali inatakiwa kuvitambua kwa kuanzisha chombo kitakachoongezea uwezeshaji wananchi wengi kiuchumi hususan wananchi wa kawaida katika maeneo ya vijijini na mijini. Usimamizi wa Baraza la Uwezeshaji unatakiwa uboreshwe zaidi kwa kulifanya Baraza liweze kusimamia kwa ufanisi zaidi shughuli mbalimbali za uwezeshaji kiuchumi na vile vile uwezeshaji kiuchumi uainishwe katika sekta zote; na

vi) Mchakato wa kuweka misingi ya uchumi imara na wenye uwezo wa kishindani unatakiwa uboreshwe kwa dhati kwa kuanzia katika maeneo yafuatayo:

- Kukibadilisha kilimo kuwa cha kisasa kwa kulenga katika masuala ya uzalishaji ikiwa ni msingi wa kuongeza kipato na kufanya mabadiliko ya kiuchumi yanayotoa kichocheo katika mapinduzi ya viwanda;
- Kuwepo na program zitakazowashirikisha wananchi wazawa katika uzalishaji mali na kumiliki mchakato huo;
- Kukuza hali ya kujiamini, kuongeza ubunifu, uvumbuzi na kuwa na jamii yenye juhudi za kufanya kazi, utaalamu na ustadi wa biashara. Vitu hivi vinaweza kutekelezwa kwa kuiwezesha jamii kuwa na utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii na kuijengea uwezo kuhimili ushindani. Hivyo, mfumo wa elimu na mafunzo unatakiwa ubadilishwe ili uweze kutimiza malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; na

- Kukuza ushirikiano wa sekta binafsi na umma (Public-Private Partnership - PPP) katika utendaji kazi katika sekta za miundombinu, huduma za jamii na nyinginezo. Kwa kufanya hivyo, zoezi linaloendelea la kuendeleza/kustawisha sera za PPP linatakiwa liende kwa haraka na pindi litakapokamilika liweze kutangazwa sambamba na utekelezaji wake na lisimamiwe kwa karibu zaidi na Tume ya Mipango.

1.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango

Tume ya Mipango imepitia na kuchambua Ripoti iliyotolewa na Mtaalamu Mwelekezi. Kimsingi Tume inakubaliana na Mapendekezo yaliyotolewa na hivyo kuna umuhimu wa kuyafanyia kazi mapema ili kufidia muda uliopotea kutokana na kuchekewa kuifanyia Dira tathimini. Tume inashauri kuanza na yafuatayo:

i) Mfumo **wa Kitaasisi. (Institutional Framework):** Tume ya Mipango iendelee na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Dira kwa kuhakikisha kuwa Dira inaeleweka vyema na kila mwananchi. Kwa kuanzia, ni muhimu Dira ikatafsiriwa kwa lugha rahisi (popular version) na jukumu la kuwaelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu Dira ya Taifa liwe ni la kila mtanzania.

i) **Mipango ya Muda Mrefu (2010 – 2025):** Suala la kuwa na Mpango wa muda mrefu wa kutekeleza Dira ni muhimu. Hivyo inapendekezwa kuwa Tume ya Mipango ianze mchakato wa kuandaa mpango wa muda mrefu 2010-2025 (miaka 15) ili kuweka bayana mwelekeo wa kutekeleza Dira. Aidha, **Mpango wa Muda wa Kati** (miaka 5) ambao utakuwa unalenga katika kutekeleza mpango wa muda mrefu ni muhimu uandaliwe. Sera, mipango, programu na mikakati yote ya maendeleo itatakiwa kuelekezwa katika kutekeleza mipango ya muda mrefu na wa kati. Ni katika mpango wa muda wa kati ambapo mipango, programu na mikakati kama: MKUKUTA, SEZ, EPZ, MPIP, Kilimo Kwanza itatekelezwa. Hii itapunguza uwezekano wa kuibuka mipango au mikakati mingine ambayo haipo kwenye mipango ya muda mrefu na wa kati na hivyo kuyumbisha mwelekeo wa utekelezaji wa

Dira 2025.

ii) **Utekelezaji** wa Sera ya ‘‘Public Private Partneship’’ unaweza kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Tume ya Mipango itafuatilia kuhakikisha kuwa utekelezaji wake unaendana na mpango wa muda mrefu na wa kati.

2.0 KUAINISHA MAENEO YATAKAYOCHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI WA TANZANIA KULINGANA NA FURSA ZILIZOPO

2.1 Chimbuko

Katika miaka ya hivi karibuni uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika kama inavyojidhihirisha katika viashiria vya uchumi jumla ambavyo vinajumuisha ukuaji wa Pato la Taifa, mwenendo wa bei na mapato ya serikali. Hata hivyo, kufuatana na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na yale ya Milenia ya kufikia kiwango cha ukuaji cha asilimia 8-10 kwa mwaka, kasi ya ukuaji wa uchumi haiashirii kufikia malengo hayo. Kiwango kikubwa cha ukuaji wa uchumi na mgawanyo sawa wa rasilimali ndiyo kipaumbele kikubwa kwa Serikali ya Tanzania na ni ufunguo wa matokeo ya mkakati wa kuondoa umaskini. Dira inatekelezwa kupitia mipango na mikakati kama MKUKUTA na "*Mini Tiger Plan 2020"*. Jitihada hizo zimekuwa zikichangia katika ukuaji wa uchumi na kuboresha utoaji wa huduma za jamii. Hata hivyo, matokeo yake siyo ya kuridhisha na hivyo kukawa na umuhimu wa kufanya utafiti ili kuainisha maeneo yatakayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kutegemea fursa zilizopo. Hivyo, Tume ya Mipango kwa kumtumia mtaalamu mwelekezi (ESRF) ilifanya utafiti wenye lengo la kuainisha maeneo yatakayochochea ukuaji wa uchumi wa Tanzania kulingana na fursa zilizopo.

2.2 Malengo

Lengo kuu la kufanya utafiti huu ni kuainisha maeneo ambayo yatachochea ukuaji wa uchumi ili kuiwezesha Tanzania kufikia Malengo ya Milenia kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

2.3 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya Utafiti umeainisha sekta tano (5) pamoja na vichocheo husika katika kukuza uchumi kwa haraka. Sekta hizo ni;

i) Kilimo – Sekta ya kilimo ilionekana kuwa na sifa kuu mbili katika kuharakisha ukuaji wa uchumi kama ifuatavyo;

- Asilimia kubwa ya watanzania (hasa wanaoishi vijijini) wanategemea kilimo kwa ajili ya ajira na kujikimu katika maisha yao; na
- Shughuli nyingi za kilimo zina mahusiano au kutegemeana na sekta nyingine (backward and forward linkages) kama vile viwanda na usafirishaji.

Aidha utafiti ulibaini vichocheo 7 muhimu (growth drivers) katika kuleta mapinduzi ya kilimo (Agricultural transformation) kama ifuatavyo;

- Miundombinu ya usafiri na usafirshaji;
- Teknolojia ya habari na mawasiliano;
- Miundombinu ya umwagiliaji maji;
- Nishati;
- Kukuza upatikanaji wa mikopo na mitaji kwa ajili ya sekta ya kilimo;
- Elimu kwa wakulima; na
- Kilimo cha biashara na uzalishaji viwandani.

ii) Uzalishaji wa **Bidhaa Viwandani** (Manufacturing) – Utambuzi wa sekta hii umetokana na mchango wake katika kulipatia Taifa mapato mengi ya kodi na kuwa na vyanzo vingi vya mapato kutokana na bidhaa zake zinazozalishwa kupitia kodi ya mapato nje, (corporate and income tax). Karibu nusu ya mapato yanayokusanywa hapa nchini hutokana na uzalishaji wa bidhaa hizo.

Katika kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na uchumi anuai (Diversification of the economy), utafiti umesisitiza muhimu wa sekta ya uzalishaji wa bidhaa viwandani kupewa kipaumbele kwa kuwa utasaidia uchumi kutotegemea sekta moja tu ya kilimo ambayo sehemu kubwa ya uzalishaji hutegemea mvua zisizotabirika. Aidha utabiri huo umeainisha sekta hii kuwa na mahusiano makubwa na sekta nyingine (backward and forward linkages) katika uzalishaji mali na hivyo upatikanaji wa ajira kwa wananchi ni mkubwa.

Utafiti ulibaini vichocheo vifuatavyo katika sekta ya uzalishaji bidhaa viwandani;

- Miundombinu bora kama vile barabara, reli, TEKNOHAMA;

- Uwepo wa nishati ya uhakika;
- Maji kwa mahitaji ya viwandani na nyumbani
- Mitaji ya uwekezaji; na
- Rasilimali watu yenye ujuzi (skilled and semi skilled).

iii) **Viwanda vidogo na vya kati (SMEs)** – Sekta ya viwanda vidogo na vya kati ni muhimu katika maendeleo ya nchi hasa kwa nchi inayoendelea kama Tanzania. Hii ni kwa sababu kuanzisha na kuendesha viwanda vidogo vidogo havihitaji mtaji au gharama kubwa, na nchi yoyote ili iweze kufikia ya viwanda vikubwa ni wazi kwamba itaanzia katika ngazi ya viwanda vidogo vidogo. Pia sehemu kubwa ya wananchi wameajiriwa au wamejiajiri katika sekta hii.

Katika sekta ya viwanda vidogo,vichocheo vilivyobainishwa ni kama vilivyoorodheshwakatika sekta ya uzalishaji viwandani.

Aidha, utafiti huo umeainisha vichocheo vinavyohusika moja kwa moja na ukuaji wa uchumi kama ifuatavyo;

- **Nishati** – Tanzania ni nchi iliyojaliwa vyanzo mbalimbali vya nishati kama vile umeme wa maji na gesi. Vikitumika kwa ufanisi vitachochea ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali.
- **Miundombinu** – Kijiografia Tanzania ni nchi ambayo imezungukwa na nchi za jirani ambazo hazipo pembezoni mwa bahari, hivyo inaweza kutumia nafasi hii kuendeleza usafiri wa majini kwa ajiri ya kutoa huduma kwa nchi jirani ambazo hazina nafasi hiyo. Pia kuwepo kwa ukanda wa usafiri wa nchi kavu kama vile Mtwara corridor kunaweza kukachochea usafirishaji wa bidhaa, watu na mali kutoka sehemu moja hadi nyingine. Usafiri unapokuwa upo katika hali nzuri inakuwa rahisi kusafirisha bidhaa au watu kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa urahisi, mfano kwa upande wa mazao kutoka sehemu ya uzalishaji mpaka yalipo masoko.

- ***Mfumo wa habari na mawasiliano*** – Mfumo wa habari na mawasiliano ni kichocheo muhimu katika kuleta maendeleo ya nchi kwa sababu hurahisisha mawasiliano na kupunguza gharama za uzalishaji, usafirishaji na muda unaopotea ni mchache katika ngazi

mbalimbali na swala zima la ushindani katika dunia.

2.4 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango

Tume ya Mipango imekubaliana na baadhi ya maeneo yaliyoibuliwa na inashauri serikali ielekeze nguvu na rasilimali zaidi katika sekta hizo ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuharakisha kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla;

Sekta hizo ni;

- Kilimo;
- Uzalishaji viwandani zikiwemo SMEs; na
- Utalii.

Aidha vichocheo muhimu kwa sekta zote ni;

- Nishati;
- Miundo mbinu ya usafirishaji;
- Maji;
- TEKNOHAMA;
- Upimaji ardhi; na
- Rasilimali watu.

Taarifa: Utafiti huu ulitakiwa ufanywe katika awamu mbili. Awamu ya pili ambayo mtaalamu mwelekezi alitakiwa kuainisha mpango kazi na gharama husika itawasilishwa kabla ya mwezi wa tatu.

3.0 UJUZI UNAOHITAJIKA KATIKA SOKO LA AJIRA KWENYE SEKTA ZA MADINI, UKARIMU NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

3.1 Chimbuko

Kwa kipindi hiki, Tanzania haina takwimu za uhakika zinazoonesha idadi na aina ya wataalamu katika ngazi mbalimbali za ujuzi hapa nchini. Utafiti wa kitaifa wa mara ya mwisho uliotathimini hali ya wataalamu nchini ulifanyika mwaka 1992. Tangu hapo, mabadiliko mengi ya kiuchumi, kijamii, na kisiasa yametokea na yamekuwa na mahitaji tofauti katika eneo la wataalamu. Kutokana na pengo la kuwa na taarifa na takwimu hizo, serikali tangu mwaka 2007 iliona umuhimu wa kufanya utafiti wa kitaifa kujua hali ya wataalamu ilivyo nchini na kuandaa Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Watumishi. Utafiti wa namna hiyo unategemewa kufanyika kwa pamoja katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Kwa vile maandalizi ya utafiti katika nchi nyingine za Jumuiya yanachukua muda mrefu, Tume ya Mipango imeona ni muhimu ifanye utafiti mdogo kwenye eneo la ujuzi katika sekta muhimu tatu zinazokua kwa kasi, ambazo ni madini, Ukarimu na TEKNOHAMA, kama sehemu ya utafiti utakaozihusisha nchi zote za Jumuiya. Kwa mantiki hiyo, mtaalamu mwelekezi (HR Consult Ltd) alichaguliwa na Ofisi hii kufanya utafiti wenye lengo la kubaini ujuzi uliopo na unaohitajika katika soko la ajira kwa kuzingatia sekta za Madini, Ukarimu (hospitality) na TEKNOHAMA.

3.2 Lengo la utafiti

Lengo kuu na la jumla la utafiti huu ni kubaini aina ya ujuzi uliopo na unaohitajika katika soko la ajira kwenye sekta tatu za kipaumbele ambazo ni Madini, Ukarimu (Hospitality) na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA).

3.3 Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtaalamu mwelekezi, ameibua mambo muhimu yafuatayo:

i) **Uwiano usio sawia kati ya wataalamu na mafundi mchundo**

Takwimu katika sekta zote tatu kwa ujumla zinaonyesha mlundikano mkubwa katika kada ya juu yaani ya wataalamu na upungufu katika kada ya kati yaani mafundi mchundo na kada ya chini. Uwiano uliojionyesha ni kama ufuatao: 1:0.8:0.3 kwa TEKNOHAMA, 1:0.8:0.3 kwa ukarimu na 1:0.9:4.3 kwa sekta ya Madini. Kwa mfano, uwiano unaotakiwa katika eneo la uhandisi ambayo haiwezi kuwa tofauti sana na sekta nyingine ni 1:5:15.

ii) **Mitaala ya kufundishia katika taasisi za elimu kisekta haiendi sambamba na ujuzi unaohitajika katika soko.**

Utafiti umeonyesha kuwa mitaala inayotumika kufundishia inatakiwa itokane na mahitaji ya waajiri (yaani kuwe na ushauri kutoka kwa waajiri na mamlaka za elimu kama vile VETA na NACTE). Lakini vyuo vingi katika sekta hizi tatu vinamilikiwa na watu binafsi na havina wataalamu wanaoweza kuainisha mabadiliko ya mitaala kulingana na mabadiliko ya soko la ajira na hali ya uchumi kitaifa, kikanda na kimataifa. NACTE na VETA ni mara chache wanafanya ufuatiliaji na hata wakifanya unakuwa haujafanyika kwa wakati unaotakiwa na hivyo hauwezi kutatua tatizo kwa wakati husika.

iii) **Kuna mahitaji makubwa ya ujuzi mpya unaoibuka**

Katika sekta zote tatu, imeonekana kuwa kuna ujuzi unaoibuka kutokana na mabadiliko ya teknolojia, mifumo ya uongozi, tamaduni za utendaji kazi na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

iv) **Uwiano usio sawa wa Jinsia katika ajira**

Sekta za TEKNOHAMA na Madini zimeonyesha idadi ndogo sana ya ajira kwa wanawake. Hali hii ni tofauti kabisa katika sekta ya Ukarimu ambako wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya ajira zote. Wanawake wachache waliopatikana katika sekta za TEKNOHAMA na Madini hawako katika sehenu za muhimu za makampuni/mashirika, wako katika nafasi za chini za wasaidizi katika ofisi za utawala, uhasibu na

ukatibu mahsusi na huduma zingine.

v) **Uhaba wa vitendea kazi na matumizi duni ya TEKNOHAMA**
Kuna upungufu wa rasilimali watu katika utumiaji mzuri, umilikaji na usimamizi wa rasilimali za TEKNOHAMA na miundombinu yake.

vi) **Mipango katika Vyuo vya Mafunzo hauoani na mipangilio ya Viwango vinavyokubalika.**
Takwimu za kupanga makundi ya rasilimali watu zinatakiwa zifuate *"Tanzania Standard Classification of Occupations"* (TASCO), ambayo hufuata utendaji wa kazi na ujuzi unaohitajika. Lakini utafiti umeonyesha kuwa upangaji huu hautumiki katika vyuo vya mafunzo.

vii) **Ukosefu wa Uwazi katika Tozo ya Mafunzo**
Kusudi la tozo ya Mafunzo ni kusaidia au kuwezesha vyuo vya mafunzo kuendesha majukumu yao vema na kutoa ujuzi unaotakiwa na wenye ushindani. Hii ni asilimia 6 ya kodi ya mishahara ya wafanyakazi wote. Kwa bahati mbaya matumizi ya fungu hili hayajulikani kwa wanaokatwa. Hii inafanya waajiri waone kama ni chanzo kingine cha mapato kwa serikali.

viii) **Upungufu katika muundo wa sasa wa Sera za Madini na Uwekezaji**
Utafiti unaonesha kuwa ajira za wageni zimejikita sana katika nafasi za juu na kati kutokana na upungufu wa kisera. Mfano Sera ya Madini inawapa wawekezaji idadi ya nafasi zozote wanazotaka bila kuweka ukomo. Kwa upande mwingine wawekezaji wanaoingia nchini kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC) wanaruhusiwa kuingiza wataalamu wa nafasi tano za juu za wataalamu. Wataalamu wa ziada wanaingia kupitia kibali maalumu cha kazi kinachotolewa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

3.4 Mapendekezo ya Mtaalamu Mwelekezi

i) Serikali iandae Mkakati wa Kuendeleza Rasilimali Watu kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025. Mkakati uainishe maeneo ya

kuwekeza katika mafunzo na viwango kwa kila kada. Mkakati lazima uonyeshe mpango wa mafunzo wa muda mfupi na mrefu katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Sekta binafsi ishirikishwe katika uandaaji na utekelezaji wa mkakati huo.

ii) Serikali itoe mwongozo wa mitaala inayotakiwa kufundishia kwa uwiano unaotakiwa. Kwa mfano baadhi ya taasisi za elimu ya juu zinaweza kuendelea na programu ya kutoa stashahada wakati huo huo ikiendelea kutoa kozi za shahada katika uwiano utakaopendekezwa ikizingatiwa kwamba uchumi unahitaji mafundi mchundo zaidi kuliko wataalamu wa ngazi za juu.

iii) Serikali iendelee na juhudi za kuwahamasisha wanawake kuchukua masomo ya sayansi ambayo yatawawezesha kusoma kozi za TEKNOHAMA. Pia paanzishwe mfuko utakaosaidia wanawake katika maeneo ya ujasiriamali na mafunzo mengine (yaani katika fani za ufundi).

iv) VETA, NACTE na TCU zifanye tafiti za mara kwa mara katika soko la ajira na kuyatoa matokeo ya tafiti hizo katika vyuo vya mafunzo. Aidha, vyuo vya mafunzo vifanye mabadiliko ya mitaala ya ufundishaji mara baada ya matokeo yenye mabadiliko katika soko la ajira kubainishwa.

v) Serikali ianzishe utaratibu utakaowezesha matumizi ya teknolojia kuwa rahisi na ya gharama nafuu. Wakati huo huo VETA na NACTE zisimamie na kudhibiti mafunzo ya TEKNOHAMA katika vyuo vinavyotoa mafunzo ili vitoe elimu bora na ya kiwango kinachotakiwa kwa watoa huduma, wakufunzi na watumiaji.

vi) Wizara inayotoa elimu ianzishe mafunzo ya kina ya elimu ya kompyuta katika shule kuanzia za msingi na kuwa na maono ya muda mrefu kufanya elimu ya kompyuta kwa wote katika kizazi hiki cha sasa na kijacho.

vii) Taasisi za Mafunzo ni lazima ziwe na uelewa wa mahitaji ya soko la ajira na aina ya kazi zitakazofanywa na wahitimu wake, ili watoe mafunzo yanayoendana na mahitaji hayo yatakayojibu tatizo la ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na wakati huo huo vianzishe upya mwongozo wa ajira na ushauri kuwawezesha wanafunzi kuwa na habari muhimu za fursa za ajira zilizopo;

viii) Mapato yanayotokana na Tozo la Mafunzo yatumike kujenga uwezo unaotakiwa wa vyuo vya mafunzo ili ipunguze gharama za mafunzo na kuwawezesha waajiri kupata nafasi za mafunzo kwa waajiriwa wao;

ix) Kufanya tathmini na kuanza kutumia sera ambazo zitahakikisha wataalam wazawa wanawezeshwa kwa lengo la kutumia teknolojia mpya. Yafuatayo yanatakiwa kufanyika;

- Kutathmini vipingamizi vinavyozuia maendeleo ya wataalamu wazawa katika sekta hizi;
- Kuendeleza na kuimarisha programu inayowapa wataalamu fursa ya kujifunza kwa vitendo kutoka kwa makampuni/mashirika mengine ndani ya nchi au nje ya nchi (exposure); na
- Kuainisha maeneo ambayo yatakuwa ya wazawa tu na vibali vya wageni visiwape nafasi wasio wazawa kupata nafasi hizo ambazo wazawa watakuwa na uwezo nazo.

3.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango

Baada ya kuchambua matokeo ya utafiti na mapendekezo ya wataalamu waelekezi kwa kuzingatia hali halisi ya sasa, Tume ya Mipango inashauri yafuatayo;

i) Serikali iaandae Mkakati wa Kuendeleza Rasilimali Watu kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na mahitaji ya sasa na ya baadaye ya soko la ajira. Aidha, Sekta binafsi ishirikishwe katika uandaaji na utekelezaji wa mkakati huo.

ii) Serikali ihuishe na kuboresha Sera ya Uwekezaji na kuharakisha mapitio ya sera ya Madini kwa kuzingatia yafuatayo;

- Sera mpya iingize kipengele kinachomtaka mwekezaji kuwawezesha wazawa kujifunza aina ya teknolojia (Technology Transfer) inayotumika. Mfumo huu umeziwezesha nchi zilizoendelea kufanikiwa kufikia maendeleo yake.
- Kuingiza kipengele kinachomtaka mwajiri awe na mpango wa mafunzo wa muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi wake. Hii itaongeza tija kwa rasilimali watu na Pato la Taifa kwa ujumla.
- Iwepo nia thabiti ya kufanya tafiti zenye lengo la kujua jinsi

ambavyo taifa letu litafaidika na rasilimali yetu ya madini.

iii) Serikali ihuishe Sera ya Elimu kwa lengo la kuzingatia yafuatayo;

- Kuhimiza mafunzo katika kada zote kulingana na mahitaji ya soko la ajira;
- Kuwepo kwa kipengele cha kuanzisha na kuimarisha kitengo cha ushauri wa kimasomo katika shule na vyuo.
- Vyuo vya Serikali na binafsi vielekezwe kuwa na mitaala inayokidhi soko la ajira; na
- kuhimiza masomo ya kompyuta kuanzia ngazi ya shule za msingi.

iv) Serikali ipanue Chuo cha Madini cha Dodoma na vingine vya aina hiyo ili kuweza kutoa wahitimu wengi katika kada ya Mafundi Mchundo na kada za juu ili nchini iweze kufaidi matunda ya madini.

v) Serikali isisitize waajiri wa makampuni/mashirika kuwapa mikataba ya muda maalumu (muda wa kati na mrefu) waajiriwa wao, badala ya kuwaajiri kama vibarua au kuwa na ajira za muda mfupi. Uhakika wa ajira unamuongezea mwajiriwa kujiamini, kuwa mwaminifu na kuwa mbunifu katika sehemu ya kazi;

vi) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi zianzishe vyuo zaidi katika sekta ya Ukarimu ili kupanua wigo wa taaluma na mchango wa sekta hiyo katika pato la taifa; na

vii) Utafiti wa kina ufanyike kwa lengo la kubaini uwiano mzuri kati ya wataalamu; mafundi mchundo na ngazi ya chini. Hii itasaidia kupunguza utumiaji mbaya wa nguvu kazi iliyopo.

4.0 MFUMO WIANISHI WA USAFIRISHAJI KWA AJILI YA KUONGEZA UFANISI NA UKUAJI WA UCHUMI

4.1 Chimbuko

Mfumo wa biashara wa kimataifa kwa kiwango kikubwa unaendana na hali ya utandawazi, ambapo katika karne iliyopita umekuwa ukitoa fursa na changamoto mpya kwa nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi hizo. Katika hali ya sasa mfumo wa usafiri na usafirishaji umewianishwa ndani ya mfumo wa uzalishaji. Pia imebainika kuwa miji endelevu na yenye mfumo wa usafiri na usafirishaji uliowianishwa hufanya vizuri katika maendeleo ya kiuchumi kwa kuwa na usafiri endelevu ambao husaidia kuvutia biashara, viwanda, uwekezaji na masuala mbali mbali ya kimaendeleo.

Hali halisi ya sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini inaonesha kuwa sekta hii imekuwa nyuma katika kuchangia kwenye uchumi wa Taifa ikiwa na mchango wa wastani wa asilimia 5.3 ya pato la Taifa kwa mwaka. Hii inatokana na kutokuwepo kwa maunganiko ya mifumo inayotumika katika uchukuzi, yaani Reli, Bandari, usafiri wa anga na Barabara. Mfumo wa upangaji na uendeshaji kwa kila njia unajitegemea na hauhusishi njia nyinginezo ili kuleta ufanisi katika uchumi.

Kwa kuzingatia tatizo la kuwa na mifumo ya usafiri na usafirishaji isiyokuwa na uwiano na yenye ufanisi mdogo katika sekta ya uchukuzi na uchumi kwa ujumla. Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Mtaalamu Mwelekezi (Chuo cha Taifa cha Usafirishaji) walifanya utafiti wenye lengo la kubaini jinsi ya kuondokana na mifumo iliyopo sasa na kuasili mfumo utakaounganisha mipango na aina zote za usafiri na usafirishaji (integrated transport system).

4.2 Malengo

Lengo kuu la utafiti ni kuanisha matatizo yatokanayo na mfumo wa sasa wa usafiri na usafirishaji na kupendekeza mfumo wa upangaji na uendeshaji wa

sekta hii ulio oanishi utakaochangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa haraka.

4.3 Matokeo ya Utafiti

Matokeo yaliyojitokeza katika utafiti huu ni kama ifuatavyo:-

i) Mchango wa sekta hii katika pato la Taifa umekuwa mdogo kutokana na kutokuwepo kwa mfumo oanishi, kukosekana uwekezaji wa kutosha na uendeshaji usioridhisha wa miundombinu iliyopo, mfano Bandari ya Dar es Salaam, Reli ya Kati na TAZARA;

ii) Mifumo ya njia za reli iliyopo nchini haina muingiliano, mfano reli ya kati ina mfumo wa 1.00m “gauge width” wakati ile ya TAZARA ina mfumo wa 1.067m. Tofauti hii inapelekea kukosekana kwa matumizi ya fursa za kiuchumi na kijamii ambazo zingepatikana kama kungekuwa na aina moja ya mfumo wa reli nchini na nchi jirani kibiashara;

iii) Kuna matumizi makubwa ya usafirishaji kwa njia ya barabara (89%) ukilinganisha na njia nyingine za usafirishaji (11%). Hali ambayo inachangia uharibifu wa miundombinu ya barabara nchini.

iv) Msongamano wa mizigo katika bandari hususan katika bandari ya Dar-es-salaam unaotokana na uhaba wa vitendea kazi na matatizo ya uendeshaji

v) Mchango mdogo wa bandari, reli na njia nyinginezo za usafirishaji kama bomba la mafuta na usafiri wa anga katika uchumi wa Taifa kutokana na kukosekana kwa mipango madhubuti na matatizo katika uendeshaji na uwekezaji mdogo wa miundombinu.

vi) Mipango ya kuendeleza miji na majiji nchini hauzingatii maendeleo ya miundombinu ya usafiri na uchukuzi.

vii) Kukosekana kwa chombo cha kisheria cha kuratibu, kuendeleza na kusimamia masuala yote ya usafiri na usafirishaji nchini na kupima

mchango wake katika uchumi wa Taifa. Ilibainika kwamba nchini Marekani kuna chombo chenye nguvu ya kisheria kinachoratibu shughuli za usafiri na usafirishaji katika Ofisi ya Rais (National Transport Advisory Board). Chombo hiki kinatakiwa kuwapo Tanzania ili kukabiliana na matatizo ya uwepo wa vyombo kama SUMATRA, TANROADS, TAA na TCAA ambavyo haviko “coordinated” na Bodi moja.

4.4 Mapendekezo yatokanayo na Utafiti

Mapendekezo ya utafiti uliofanyika ni kama ifuatavyo:

i) Mfumo wa usafiri na usafirishaji na uchukuzi kitaifa uboreshwe kama ilivyopendekezwa katika Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Usafirishaji (Transport Sector Investment Programme) ili uwezeshe sekta ya uchukuzi kukidhi mahitaji ya nchi.

ii) Uharakishaji wa kutekeleza sera ya PPP (Public Private Partnership Policy) ili kuharakisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika maendeleo ya miundombinu ya uchukuzi, na uendeshaji wake.

iii) Bandari, Reli na usafirishaji wa mafuta zifanye kazi chini ya taasisi moja ili kurahisisha uratibu wake. Hii itasaidia kuongeza usalama wa mizigo na kupunguza gharama za usafirishaji.

iv) Kuanzishwe reli za abiria (commuter rail transport) katika majiji husuan jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari sambamba na aina nyinginezo za usafiri kama matumizi ya boti.

v) Kuwe na miongozo itakayotumika katika kupanga miji na majiji nchini (Master Plans of Cities and Towns) inayozingatia mipango na uendeshaji miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

vi) Kuundwe chombo chenye nguvu kisheria cha kuratibu shughuli za usafiri na usafirishaji katika Ofisi ya Rais (National Transport Advisory

Board). Chombo hicho kipewe jukumu la kusimamia mapendekezo yote yaliyotolewa katika utafiti huu. Kwa mfano nchini Marekani kipo chombo kama hicho kinachoratibiwa katika Ofisi ya Rais.

4.5 Maoni ya Tume ya Mipango

Tume ya Mipango imepitia na kuchambua Ripoti ya Mtaalamu Mwelekezi ina mapendekezo yafuatayo:-

i) **Mfumo wa Kitaasisi (Institutional Framework)**

- Kiundwe chombo chenye nguvu kisheria katika Ofisi ya Rais kitakachoratibu mipango na kusimamia shughuli za usafiri na usafirishaji kwa kushirikiana na sekta husika kwa mfano wa chombo kama hicho nchini Marekani.

- Iundwe pia taasisi itakayokuwa inaratibu na kusimamia usafiri wa majini, reli na usafirishaji wa mafuta kwa pamoja ili kurahisisha mipango na uwekezaji wa miundombinu na kuhakikisha usalama wa mizigo. Uratibu huu utapunguza gharama za usafirishaji na kuongeza tija.

ii) **Utekelezaji wa sera ya Public Private Partnership (PPP)**

Utekelezaji wa sera ya PPP kuhusu uwekezaji na uendeshaji wa masuala ya usafirishaji ufanyike haraka na kwa umakini. Aidha Serikali iweke mazingira ya kuvutia uwekezaji na pia kusimamia utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP.

iii) **Utekelezaji wa Mipango ya Kupunguza Tatizo la Usafiri Mijini**

Mwongozo uandaliwe wa kuelekeza waandaaji na watendaji wa Miji, Majiji na Halmashauri za Wilaya kuwa katika mipango ya kuendeleza miji yao izingatie mipango ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

iv) **Usafiri wa Anga**

Usafiri wa anga na miundombinu yake viboreshwe kwa kuongeza uwekezaji wa vyombo vya usafiri wa anga na pia kukarabati kwa wakati na kujenga viwanja vya ndege.

5.0 MCHANGO WA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA UCHUMI WA TAIFA

5.1 Chimbuko

Katika karne ya 21 nchi zinazoendelea zinakumbana na changamoto mbalimbali, kutokana na uchumi wa dunia kutegemea upatikanaji wa haraka wa taarifa na mawasiliano kutoka sehemu moja hadi nyingine. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) ni nyenzo mpya katika dunia ya sasa na inaweka misingi ya ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali. Hata hivyo, kwa hapa Tanzania, fursa za TEKNOHAMA hazijaweza kutumika ipasavyo. Hivyo basi, Tume ya Mipango kwa kumtumia mtaalamu mwelekezi (Data Works Associates Ltd) ilifanya utafiti wenye lengo la kubaini mchango wa TEKNOHAMA katika uchumi wa Taifa.

5.2 Lengo

Kuchambua na kubaini mchango wa TEKNOHAMA katika uchumi wa Taifa na kuibua mikakati ya kuongeza matumizi mapana ya teknolojia hiyo katika uchumi wa Taifa.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti umebainisha mambo yafuatayo:

i) Sera ya TEKNOHAMA ya mwaka 2003 bado inakidhi mahitaji ya sekta hii kwa sasa.

ii) Tanzania bado iko nyuma ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki katika maendeleo ya TEKNOHAMA hasa katika uwekezaji kwenye miundombinu, mafunzo na utawala;

iii) Miundombinu ya TEKNOHAMA iliyopo haijaunganishwa hata katika taasisi moja jambo linalosababisha muingiliano katika uratibu wa njia na viwango;

iv) Masuala ya TEKNOHAMA yanasimamiwa na Wizara mbili ambazo ni Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo hivyo kuwepo kwa mapungufu katika uratibu;

v) Hakuna taasisi maalum inayoendeleza na kuongoza mafunzo ya TEKNOHAMA katika Tanzania;

vi) Hakuna mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa masuala yanayohusiana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;

vii) Mfumo wa kisheria uliopo hautoi mwongozo na maelekezo pale linapojitokeza tatizo la matumizi mabaya ya TEKNOHAMA (Cyber Crimes). Mfano mbinu gani za kukabiliana na matukio ya wizi wa kutumia mitandao ya kompyuta;

viii) Tanzania haina Mpango kabambe (Master Plan) unaoweza kufafanua majukumu ya wadau mbalimbali katika kuendeleza na kutumia TEKNOHAMA;

ix) Kutotumika lugha ya Kiswahili katika matumizi ya TEKNOHAMA; na

x) Hakuna takwimu zinazoonyesha mchango wa TEKNOHAMA katika Pato la Taifa na uwekezaji unaofanyika katika kuendeleza sekta hii.

5.4 Mapendekezo yaliyotolewa na watafiti

Wataaalamu waelekezi walipendekeza yafuatayo;

i) Kuimarisha na kuendeleza Serikali Mtandao (e-government);

ii) Kianzishwe chombo kitakachoratibu na kusimamia kuunganishwa kwa mtandao wa miundombinu ya taifa ya mawasiliano (*National* Communication *Infrastructure backbone network)* na mitandao mingine ya TEKNOHAMA;

iii) Kianzishwe chombo maalumu cha kuratibu na kuendeleza Mtandao wa Sekta Binafsi (e- private sector);

iv) Itungwe sheria ya masuala ya TEKNOHAMA pamoja na kuzipitia sheria na taratibu zilizopo.

v) Kuandaa Mpango kabambe wa TEKNOHAMA

vi) Kuanzishwa vituo vya TEKNOHAMA katika maeneo ya vijijini; na

vii) Kutumia lugha ya Kiswahili katika matumizi ya TEKNOHAMA.

5.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango

Tume ya Mipango imepitia na kuchambua ripoti iliyotolewa na mtaalamu mwelekezi na tunapendekeza yafuatayo;

A. Mapendekezo ya muda wa kati:

i) Kianzishwe chombo;

- Kitakachoratibu na kusimamia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
- chombo maalumu cha kuratibu na kuendeleza Mtandao wa Sekta Binafsi (e- private sector);

ii) kuandaliwa kwa Mpango Kabambe wa TEKNOHAMA.

B. Mapendekezo ya muda mrefu ni pamoja na:

i) kuandaa mfumo wa tathimini na ufuatiliaji; na

ii) kutungamanisha (mainstreaming) masuala ya TEKNOHAMA katika ngazi zote ili kuwa na jamii inayopashana habari na elimu kwa urahisi-.